THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

SCHOOL BASED ASSESSMENT

KISWAHILI
SEHEMU B

(For Regular Learners and Learners with Physical Disability)

Gredi ya 5 – 2026

JINA LA MWANAFUNZI : _____**GREDI :**_____

NAMBARI YA TATHMINI:_____

TAREHE:_____

JINA LA SHULE: _____

KWA MATUMIZI YA MTAHINI

JEDWALI LA ALAMA

	ZOEZI : 3 **UFAHAMU WA KUSOMA**	**ZOEZI : 4** **SARUFI**	**ZOEZI : 5** **KUANDIKA**
Swali	**1-16**	**17-30**	**31**
Upeo	**16**	**14**	**10**
Alama za mwanafunzi			
Kiwango Cha Utendaji			

Tathmini hii ina kurasa 9 zilizopigwa chapa.

Geuza ukurasa

©2026 The Kenya National Examinations Council

ZOEZI 3:UFAHAMU WA KUSOMA

Swali la 1 hadi la 4
Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Nyuma ya nyumba ya akina Amina kuna bustani ndogo. Bustani hiyo imetunzwa vizuri. Kipande hiki kidogo cha shamba kimepandwa aina nyingi za mboga. Kuna sukumawiki, kabeji, spinachi, karoti na hata mchicha.

Kila siku, Amina huamka asubuhi na mapema. Kabla ya kwenda shuleni, yeye huwasaidia wazazi wake kunyunyizia mboga hizo maji. Pia, siku ya Jumamosi, Amina hushirikiana na mama yake kupalilia na kuondoa magugu yaliyomea ili yasiharibu mboga hizo. Mama yake humshauri kila mara kuwa mgaagaa na upwa hali wali mkavu.

Anaporudi kutoka shuleni, Amina humsaidia mama yake kuchuma mboga zilizo tayari. Mama yake huziuza mboga hizo katika kibanda alichojenga karibu na nyumba yao. Nyingine, wao hutumia nyumbani.

Majirani nao hupenda mboga hizi. Huzinunua kwa wingi. Wao husema kuwa mboga huwasaidia watu kuwa na **siha** njema. Amina na mama yake hufurahia hela wanazopata kutokana na kuuza mboga. Hela hizi zinawasaidia kutosheleza mahitaji yao.

1. Kulingana na aya ya kwanza, bustani ndogo ya akina Amina inatumiwa kufanya nini?_____.

2. Kulingana na aya ya pili, mama yake Amina ni mlezi mwema kwani _____.

3. Unadhani mama yake Amina hutumia pesa anazopata baada ya kuuza mboga kutosheleza mahitaji gani?

4. “Wao husema kuwa mboga hizo huwapatia **siha** njema.” Maana ya **siha** ni _____

 ©2026 The Kenya National Examinations Council

Swali la 5 hadi la 8

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

(*Ni siku ya mashindano ya Tamasha za muziki katika kaunti ya Mamboleo. Chaninga na Zuri wamekutana nje ya ukumbi kunakofanyika mashindano hayo.*)

Zuri : Hujambo Chaninga?

Chaninga : Sijambo Zuri.

Zuri : (*Kwa furaha*.) Naomba kuwapongeza. Mmefanya vizuri sana katika tamasha za muziki. Timu yenu imepata ushindi.

Chaninga : (Akitabasamu.)Asante sana. Tulifanya mazoezi kwa bidii. Tunafurahia ushindi wetu. Kwa kweli, anayejitahidi hufaidi.

Zuri : Hakika. Kila timu ilijitahidi. Lakini hebu nieleze siri ya ushindi wenu.

Chaninga : (*Akichangamka zaidi*.) Kama nilivyosema hapo awali, tulitia bidii kama ya mchwa. Aidha, tulichagua mapambo yaliyofaa kwa ngoma yetu ya asili.

Zuri : (*Akimakinika*.) Enhe! Mapambo gani ?

Chaninga : (*Akiashiria*.) Tulivaa mikufu, kidani na ushanga. Haya yalifanya maleba yetu **yavutie** sana.

Zuri : (*Kwa hamu zaidi.*) Je, mikononi na miguuni mlivaa chochote?

Chaninga : (*Akiashiria.*) Mikononi tulivaa bangili na pete zikaongeza uzuri wa mavazi yetu. Miguuni tukavaa njuga. Tulipocheza njuga hizo zilitoa sauti zilizowapendeza wakaguzi pamoja na watazamaji.

 ©2026 The Kenya National Examinations Council

Zuri : Bila shaka mapambo hayo yalifanya timu yenu ionekane maridadi na yenye kujiamini jukwaani. Hiyo ndiyo maana mliibuka washindi na kuwabwaga wapinzani wenu. Hongera kwa timu nzima.

Chaninga : Asante sana.

(*Wanaondoka na kurudi ukumbini kuendelea kutazama mashindano.*)

5. Zuri anampongeza Chaninga kwani

   .....

6. Ni nini kilichoifanya timu ya akina Chaninga kupata ushindi?

   .....

7. Je, unadhani mapambo waliyovaa akina Chaninga yalikuwa yametoka wapi ?

   .....

8. Neno **yavutie** limetumika katika kifungu. Maana yake ni

   .....__

Swali la 9 hadi la 12
Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Hapo zamani za kale, Sungura na Fisi walikuwa marafiki wa dhati. Waliishi katika kijiji kimoja na wanyama wengine. Ilikuwa desturi ya wanyama kuandaa mashindano ya kucheza densi. Wanyama walioibuka washindi walitunukiwa zawadi. Sungura na Fisi

walishiriki mashindano hayo na wakaibuka washindi. Kila mmoja wao alipewa kitita cha pesa.

Fisi alifurahi sana. Aliona kuwa alikuwa amepata nafasi nzuri ya kufurahia maisha. Alitumia pesa zake kiholela bila mpango wowote. Baada ya siku chache, fedha zote ziliisha. Alibaki maskini hohehahe. Hakuwa na mbele wala nyuma. Kazi yake ikawa ni kulala usiku na mchana.

Sungura naye aliwaza na kuwazua kabla ya kutumia hela zake. Aliamua kununua mizinga miwili ya nyuki na vifaa vya kutunzia nyuki. Aliweka mizinga hiyo mahali salama kwenye miti yenye maua mengi. Nyuki walizalisha asali. Sungura alivuna asali nyingi. Akaitia kwenye vichupa vidogo vidogo. Aliiuza sokoni. Asali iliyobaki aliwauzia wenye maduka humo kijijini.

Fedha ambazo Sungura alipata aliongeza mizinga mingine ya nyuki. Biashara yake **ilinawiri**. Aliweza kujenga nyumba nzuri na kuwasomesha watoto wake. Pia, alimsaidia Fisi pamoja na wanyama wengine waliokuwa na matatizo. Hakika, Sungura alikuwa mfano mzuri wa kuigwa katika jamii.

9. Kulingana na kifungu, Sungura na Fisi walipata pesa zao vipi?

   .....

10. Sungura aliwaza na kuwazua kabla ya kutumia hela zake. Hili linaonyesha kuwa Sungura ni .....

11. Unadhani Fisi alifanya nini ili kubadilisha hali yake ya maisha?

    .....

12. Neno, **ilinawiri** limetumika katika kifungu. Maana yake ni .....

 ©2026 The Kenya National Examinations Council

Swali la 13 hadi la 16

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Wakati wa likizo ya Disemba, Bob na kaka yake Juma walienda kumtembelea babu yao kijijini. Babu yao ni mkulima hodari. Babu aliwakaribisha kwa furaha. Baada ya kupumzika, Babu aliwapeleka shambani. Huko, aliwaonyesha mimea mbalimbali. Miongoni mwa mimea aliyowaonyesha ni miembe, mipera na michungwa.

Babu aliwaeleza kuwa baadhi ya mimea hiyo huwa dawa, mingine huzaa matunda yanayoliwa, na mingine hutoa kivuli. Aliwaambia kuwa miti hutoa hewa safi.

Baada ya kuzuru shamba lote, Babu aliwaelekeza kulikokuwa miche. Aliwapa miche ya miembe na miparachichi na kuwaonyesha namna ya kuipanda. Bob na Juma walipanda miche hiyo. Baada ya kuipanda, waliinyunyizia maji. Walifurahia kunyunyizia miche maji. Walijua kuwa miche waliyopanda ingewaletea matunda mengi baadaye. Aidha, Babu aliwaonyesha namna ya kupalilia na kuwekea mimea mbolea ili ikue vizuri. Kisha walienda kuchuma machungwa yaliyoiva. Waliyaweka kwenye kikapu kwa makini na kuyapeleka nyumbani. Waliyala kwa furaha. Kila siku, Bob na Juma walipata fursa ya kutembea shambani na babu yao.

Baada ya likizo kukamilika, walirejea nyumbani. Waliwasimulia wazazi wao kuhusu likizo hiyo. Hawakusahau kuwaeleza **manufaa** ya mimea kama walivyofunzwa na babu yao. Waliwaomba wazazi wao wanunue miche ya matunda ili nao waweze kuipanda kama anavyofanya babu yao kijijini.

13. Kwa nini Babu aliwapeleka Bob na Juma shambani walipomtembelea?

    .....

14. Ni jambo gani linaloonyesha kuwa Babu anafahamu jinsi ya kutunza mimea?

    .....

 ©2026 The Kenya National Examinations Council

15. Je, unafikiri Bob na Juma walifanyia nini matunda waliyopata baada ya mimea yao kukomaa?

.....

16. Neno, **manufaa** limetumiwa katika kifungu. Maana yake ni.....

ZOEZI 4: MATUMIZI YA LUGHA

17. Jozi ni nomino ya makundi. Mafuta ni nomino ya .....

18. Chagua jibu sahihi kujaza nafasi katika sentensi ifuatayo:
Mchezo huo ..... mashabiki wengi. (ulivutiwa, uliwavutia)

19. Geuza sentensi ifuatayo iwe katika hali ya umoja.
Teo hizo zimeundwa vizuri.
.....

20. Jaza nafasi katika jedwali. Fuata mfano.

Kiatu cha mtoto huyu kinametameta.	Kijiatu cha kitoto hiki kinametameta.
Mkia wa mbuzi huyu una madoadoa.	.....

21. Kanusha sentensi ifuatayo.

Wasanii wamejiandaa kwa sherehe hiyo.

.....

22. Neno, **zao** katika sentensi, **Bidhaa zao ziliwavutia wengi** ni kivumishi.

Pigia mstari kiwakilishi katika sentensi hiyo.

23. Akifisha sentensi ifuatayo:

Juma Rehema Roda na Hamisi walimsaidia shangazi kufuma mkeka

.....

24. Nomino **kikapu** iko katika ngeli ya KI-VI. Je, nomino **nyumba** iko katika ngeli gani?

.....

25. Pigia mstari kielezi katika sentensi ifuatayo:

Wauguzi walimhudumia mgonjwa akapona haraka.

 ©2026 The Kenya National Examinations Council

26. Chagua neno sahihi kujaza nafasi katika sentensi ifuatayo:

    Katika msimu wa masika, shamba ..... vizuri. (hulimiwa, hulimika)

27. Barabara ni kwa baraste ilhali ndovu ni kwa.....

28. Andika sentensi ifuatayo katika wakati uliopo.

    Katoo atasafisha chumba chake mapema.

    .....

29. Akiba haiozi ni methali. Tengana kama ardhi na mbingu ni.....

30. Timu yako imeshinda mechi kwa mara ya pili. Andika kihisishi utakachotumia kujaza nafasi ifuatayo:

    ..... Tumeshinda tena.

ZOEZI 5: KUANDIKA

31. Rafiki yako ni mwimbaji hodari. Anasifika sana shuleni mwenu. Andika insha ya wasifu kumhusu.

 ©2026 The Kenya National Examinations Council

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.

©2026 The Kenya National Examinations Council